



Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

Somo la 51 Ahadi za Mungu kwako

SOMA Habakuki 2:14; Kutoka 33:18 – 19 & 34:6 – 7;
Mwanzo 1:26 – 27 & 3:15 & 12:2 – 3; 2 Samwelii 7:12 – 13; Isaya 11:1 – 9

SOMO

Mungu anatwambia sababu ya kuumba dunia. "Kwa maana dunia itajazwa maarifa ya utukufu wa Bwana, kama maji yafunikavyo bahari." Habakuki 2:14. Kusudi ya Mungu ni kwamba dunia itajazwa maarifa ya utukufu Wake.

Utukufu wa Mungu ni tabia zake ya maana na ajabu. Kwa hivyo kusudi ya Mungu ni kujaza dunia na watu wanaojua utukufu wake. Ni watu wanaonyesha tabia zake katika maisha yao.

Kusudi ya Mungu ikisha malizika, watu wote duniani watakuwa na tabia za Mungu. Hii ndiyo kusudi Mungu ako nayo na dunia. Mungu anaita watu wampende na wamtii ili wawe kwa Ufalme wake hapa duniani.

Mungu aliumba mtu kwa sura yake na mfano wake. (Mwanzo 1:26 – 27). Tangu mwanzo Mungu alitaka mwanadamu ampende na kupenda kwake aonyeshe tabia yake ya ajabu katika maisha yake. Adamu na Hawa waliharibu mpango wa Mungu. Hawakupenda Mungu kamili. Hawakutii Mungu.

Mwanadamu aliharibu kusudi ya Mungu kwa muda. Lakini hata hivyo kusudi ya Mungu itafaulu. Mungu amekuwa akifanya hii kusudi ikuweko kutoka mwanzo. Mungu amefanya ahadi kwa watu waimani akiwambia vile atatimiza kusudi yake kwa dunia. Mungu atasimamisha Ufalme wake hapa duniani. Dunia itajazwa na utukufu wake.

Mungu aliahidi ahadi za tumaini ya kuonyesha wanaume na wanawake kwamba ataendelea kufanya hilo kusudi kwa dunia.



Maswali na Majibu

1. Mbona Mungu aliumba nchi?
Kujaza nchi kwa utukufu Wake.
2. Utukufu wa Mungu ni nini?
Utukufu wa Mungu ni tabia Zake za ajabu.
3. Mpango wa Mungu uliharibikaje?
Wakati Adamu na Hawa walifanya dhambi kwa kutomtii Mungu.
4. Mpango wa Mungu umeharibika milele?
Hapana. Mungu alifanya ahadi za tumaini juu ya kusudi yake kwa nchi.
5. Mungu alifanya ahadi kwa kina nani?
Adamu na Hawa, Ibrahimu, Daudi.
6. Nani alitimiza hizi ahadi zote? *Yesu.*
7. Hizi ahadi za Mungu zilikuwa kwa taifa gani? *Wayahudi.*
8. Sisi tunaweza kuwa na sehemu kwa hizi ahadi namna gani?
Kupitia kwa ubatizo.
9. Yesu atakaporudi atatawala kama Mfalme kutoka wapi?
Yerusalemu
10. Nchi itakuwa namna gani wakati kusudi ya Mungu itakapotimizwa?
Itajazwa kwa maarifa ya utukufu Wake.

Mistari ya kukariri

Habakuki 2:14 Isaya 2:4 Isaya 11:6

Mazungumzo

Zungumza vile mwanadamu aliharibu mpango wa Mungu, ingawaje kusudi yake itatimizwa. Zungumza juu ya ahadi zenyenye Mungu alifanya. Zinatimizwa na Yesu namna gani? Zitatimizwa sawasawa namna gani kwa Ufalme?

Kuandika

Eleza vile Ufalme wa Mungu utakuwa.

MUNGU ALIAHIDI

Adamu na Hawa mzao wa kipekee atakaeokoa watu kutoka kwa dhambi zao, na kuleta ushirika mpya na Mungu.

Ibrahimu watu - Wayahudi
nchi - nchi ya Israeli
mzao wa kipekee atakayeleta ahadi za Mungu kwa watu wote ulimwenguni

Daudi mzao wa kipekee atakayekuwa Mfalme kwa kitu cha enzi kule Yerusalemu. Atatawala ulimwengu

Hizi ahadi zote zinatimizwa na Yesu Kristo

Yesu alikuja kutimiza ahadi za Mungu zote. Yesu aliyeana uhai wake usiokuwa na mawaa wakati alisulibwa. Yesu aliharibu nguvu za dhambi na kifo. Kupitia kwa ubatizo katika Yesu, tunaweza kusamehewa dhambi zetu na tuwe kwa ushirika na Mungu. Tunaweza kuwa na sehemu kwa ahadi za Mungu.

Yesu alifufuliwa kutoka kwa wafu. Alienda kuishi na Mungu Mbinguni. Hivi karibuni Yesu atarudi hapa duniani tena. Yesu atafufua wafu. Atahukumu watu kulingana na vile wamekaa maisha yao. Atapea uzima wa milele kwa wale walioishi kwa imani. Uzima wa milele ni uhai usio wa kawa. Watu watakapata uzima wa milele hawatatenda dhambi tena. Watakuwa na tabia kama za Mungu. Watakuwa na hekima na maarifa ya juu. Hawatakuwa na njaa wala kuchoka au kugonjwa. Hawatakuwa na huzuni wala maumivu. Wataishi milele kwa Ufalme wa Mungu. Watasaidia Yesu kutawala ulimwengu.

Yesu atakuwa mfalme Yerusalemu. Atatawala nchi zote za ulimwengu. Yerusalemu iko katikati ya ulimwengu. Yesu atatawala na sheria za Mungu. Ni sheria zilizohaki. Sheria za Mungu zitaleta amani na haki.



Sheria za Mungu zitafundisha watu kuishi pamoja kwa uaminifu na kwa amani. Watoto atajifunza kumpenda na kumtii Mungu. Hakutakuwa na ufisadi na kula hongo. Hakutakuwa na vujo wala vitisho. Hakutakuwa na vita. Watu watajifunza kupendana na kuishi kwa amani. Watajifunza kuwa wakulima wazuri sio kupigania mashamba. Kutakuwa na mavuno mengi ya kutosha watu wote.

Laana iliyowekwa kwa ardhi kwa ajili ya Adamu itaondolewa. Miiba na michongoma haitakua. Mungu atabariki nchi yote na mvua ya kutosha. Hakutakuwa na jangwa wala nchi kame. Mungu ataibariki nchi na kuifanya izae zaidi. Mimea itakua hata penye kuna jangwa. Kila mwaka kutakuwa na mavuno mazuri. Hakutakuwa na njaa. Kila mtu atakuwa na chakula cha kutosha.

Kila mtu atakuwa na shamba lake la kulima. Watu watakuwa na nguvu na afya nzuri. Kila mtu atakuwa na kazi yake ya kufanya. Watafurahia kazi yao na kutosheka na wanachofanya. Watapata chakula cha kutosha familia zao. Kila mtu atakuwa na chakula na nguo na makao yake.

Chakula cha kutosha na maisha mazuri itafanya watu wawe na afya. Magonjwa na maradhi yoyote itatibiwa. Vipofu, viziwi na walemavu wataponywa. Kila mtu atafurahi na kuishi kwa amani. Hata wanyama wataishi kwa amani. Kila mtu atapenda na kumsifu Mungu.

**“Dunia itajaa na maarifa ya utukufu wa Bwana,
kama maji yafunikavyo bahari.”**

Halafu kusudi ya Mungu na dunia yote itatimizwa.

Mungu alikuwa na ahadi za kipekee kwa watu wake. Hizi ahadi zilikuwa juu ya wokovu. Zilikuwa ahadi za kuishi milele kwa Ufalme wa Mungu hapa duniani. Ahadi za Mungu zilikuwa kwa Wayahudi, watu wa Mungu. Ahadi za Mungu zote zilitimizwa kwa Yesu. Kupitia kwa kifo na kufufuka kwake, Yesu alileta wokovu kwa watu wote. Sisi ni watu wamataifa. Tunahuzishwa na kifo na kufufuka kwa Yesu kupitia kwa ubatizo. Kupitia kwa ubatizo tunakuwa na sehemu kwa ahadi zake. Tuko na tumaini la uzima wa milele kwa Ufalme Wake.

Mungu anataka tuwe kwa Ufalme Wake. Kusudi ya Mungu kutoka mwanzo ni kwamba tuwe na sehemu kwa Ufalme Wake wa ajabu hapa duniani. Mungu anatukupenda. Mungu amepeana Mwanawewe wa pekee ili tuokoke. Mungu amepeana ahadi za tumaini.